UTANGULIZI

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar imeanzishwa kwa sheria Nam. 2 ya mwaka 1998 na kufanyiwa marekebisho kadhaa na kuanzishwa upya kwa sheria Na.2 mwaka 2005 baada ya mapitio makubwa.

MADHUMUNI YA ZSSF

Madhumuni ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) ni kuwarejeshea wanachama wake uwezo wa mapato pale ambapo hawawezi kufanya kazi kutokana na majanga mbali mbali. ZSSF itamlipa kwa mkupuo (kiinua mgongo) na pia itakuwa ikiendelea kumlipa mwanachama kila mwezi (pencheni) baada ya kustaafu au kupata ulemavu hadi kufariki kwake.

KAZI ZA ZSSF

Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha sheria ya ZSSF Na.2 ya 2005 Mfuko utafanya kazi kadhaa zikiwemo:-

- Kusajili waajiriwa wote kuwa wanachama wanufaika na waajiri wote kuwa wanachama wachangiaji.
- Kukusanya michango ya wanachama wake na fedha zote zinazolipwa ZSSF.
- Kuanzisha na kuhifadhi kumbukumbu za kila mwanachama zinazohusu michango yake.
- Kuwekeza fedha zote zinazotokana na michango kwenye miradi yenye faida kama itakavyoidhinishwa na Bodi ya Wadhamini ya ZSSF
- Kufungua na kuendesha hesabu zake za benki kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa na Bodi ya Wadhamini ya ZSSF.
- Kulipa mafao kwa wanachama wake au wategemezi wa wanachama wake kulingana na Sheria ya ZSSF.
- Kudhibiti na kuendeleza michango kulingana na maelekezo ya Sheria ya ZSSF.

MAFAO YA ZSSF

Umuhimu wa kuanzisha utoaji wa mafao ya ZSSF ni pamoja na:-

- Kuendeleza jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kutoa Ustawi bora kwa wananchi wake kabla au baada ya utumishi.
- Kutimiza matakwa ya kisheria kama yalivyoainishwa katika Sheria ya ZSSF nambari 2 ya mwaka 2005.

Kifungu cha 5 cha Sheria Na. 2 ya mwaka 2005 ya ZSSF kinafafanua ulipaji wa mafao. Mafao hayo ni haki ya kila mwanachama. Mafao yapo ya muda mrefu na muda mfupi. Mafao ya muda mrefu ya ZSSF ni Mafao ya Uzeeni na Mafao ya Ulemavu ambapo mafao ya muda mfupi ni mafao ya urithi, matibabu na mafao ya uzazi. Mafao ya Upotevu wa Ajira na Mafao ya Fidia kwa kuumia kazini.

MAFAO YA UZAZI

Mafao haya yametajwa katika sheria ya ZSSF yenye lengo la kumkinga mwanachama mwanamke na majanga mbalimbali yatokanayo na uzazi au wakati ambao amekaa nyumbani akimlea mtoto wake mchanga.

Mafao haya yatamsaidia mama kuziba pengo la kipato kutokana na kutokuwepo kazini au kutokana na kutofanya kazi za ziada.

Aidha mafao haya husaidia huduma za matibabu kwa mama mjamzito au aliyejifungua pamoja na mtoto wake mchanga pindipo yanapotokezea matatizo ya afya.

Sifa zinazostahiki

Kila mwanachama mwanamke atastahili na atakuwa na haki ya kulipwa mafao ya uzazi kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kama ilivyoelezwa katika sheria baada ya kutimiza sifa na masharti yaliyowekwa katika kanuni hizi :-

(i) Awe mwanachama mwanamke aliesajiliwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar na (ZSSF) kuwa mwanachama mnufaika.

(ii) Awe amechangia katika Mfuko kwa kipindi kisichopungua miezi thelathini na sita (36), kabla ya kujifungua, au kabla ya kuomba mafao na miezi sita (6) katika miezi 36 iwe imechangiwa mfululizo karibu na wiki ya kujifungua au baada ya kujifungua.

(iii) Baada ya Mkurugenzi Mwendeshaji kupokea taarifa ya maandishi au cheti cha hospitali kilichotolewa na daktari anayetambulika kinachothibitisha kwamba mwanachama amejifungua.

(iv) Kila baada ya kipindi cha miaka mitatu (3) kutoka kipindi mwanachama alichopokea malipo ya mwisho ya Mafao ya Uzazi isipokuwa:-

(a) Mwanachama ambae atajifungua na mtoto wake kufariki ndani ya kipindi cha miezi sita (6) ya mwanzo kutoka siku aliyojifungua, au

(b) Mwanachama ambae atajifungua mtoto ambae amefariki akiwa tumboni"still birth".

(v) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ya 5(1) ya kanuni za mafao ya uzazi, mwanachama ambae atakuwa anaomba mafao ya uzazi akiwa amejifungua mtoto wa pili na kuendelea atapaswa kulipwa mafao hayo iwapo atakuwa amechangia miezi ishirini na nne (24) ya kuchangia au michango ya miezi ishirini na nne (24) kutoka mara ya mwisho alipopata mafao ya uzazi.

MAFAO YA UZAZI YANAYOTOLEWA

Mwanachama atakaetimiza sifa na masharti yaliyoelezwa katika kanuni hizi atalipwa mafao ya uzazi ikiwa ni fedha taslimu (martenity cash benefits).

Mfuko utalipa mafao ya uzazi kwa mwanachama katika kiwango cha wastani wa asilimia 30% ya mshahara wa wanachama wote wa Mfuko kwa mwezi.

Malipo ya Mafao ya Uzazi yatalipwa kwa mwanachama kwa njia ya hundi au moja kwa moja katika hesabu ya benki ya mwanachama au kwa njia nyingine yoyote ambayo Mkurugenzi Mwendeshaji ataona inafaa.

Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ya mafao ya uzazi, hesabu halisi ya kiwango cha mafao ya mwanachama kitapatikana baada ya kukokotoa mafao hayo kwa kutumia kigezo cha wastani wa mshahara wa mwezi wa wanachama wote wa Mfuko utakaotangazwa kutumika kukokotoa mafao ya uzazi kwa mujibu wa fomula iliyowekwa katika kanuni hizi.

Mfuko unaweza kuanzisha na kulipa mafao ya uzazi katika mfumo mwingine usiokuwa wa fedha taslimu kwa kadri utakavyoona kuwa inafaa kulingana na uwezo wa Mfuko kwa wakati huo baada ya kufanya tathmini ya uhai wa Mfuko.

MUDA WA MALIPO YA MAFAO YA UZAZI

Mafao ya uzazi yatalipwa kwa mwanachama katika muda ufuatao:-

(a) Kabla ya mwanachama kujifungua na/au
(b) Baada ya mwanachama kujifungua.

Mfuko utafanya malipo ya mafao ya uzazi kwa mwanachama baada ya kukamilisha taratibu za maombi zilizoelezwa katika kanuni hizi kwa awamu tatu.

Malipo ya Mafao ya Uzazi yatalipwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza yataombwa kabla ya mwanachama kujifungua. Na awamu ya pili yataombwa baada ya mwanachama kujifungua. Mwanachama ambae ataomba malipo ya mafao ya uzazi kabla ya kujifungua atapaswa kuomba mafao hayo katika kipindi kisichopungua wiki ya ishirini na nane tokea alipopata ujauzito yaani kuanzia miezi 7 ya ujauzito.

Maombi ya mafao ya uzazi baada ya kujifungua yatalipwa ndani ya kipindi cha siku tisini (90) baada ya mwanachama

kujifungua.

UTARATIBU WA MAOMBI YA MAFAO YA UZAZI

Mwanachama atawasilisha maombi ya mafao ya uzazi kabla ya kujifungua au baada ya kujifungua kwa kujaza fomu maalum ya maombi ya mafao ya uzazi Na.SSF 13 na ataambatanisha vielelezo vinavyotakiwa.

Kwa maombi ya mafao ya uzazi kabla ya kujifungua mwanachama atawasilisha zielelezo zifuatazo:-

(i) Barua ya maombi ya mafao ya uzazi.
(ii) Kadi ya Uanachama wa Mfuko.
(iii) Kivuli cha gamba la kliniki la mama.
(iv) Picha moja ya aina ya pasi ya kusafiria.
(v) Hati nyingine zozote zinazoweza kuthibitisha maombi hayo.

Baada ya uwasilishaji wa vielelezo hivyo mwanachama atajazishwa fomu ya maombi na afisa husika.

Kwa maombi ya mafao ya uzazi baada ya kujifungua mwanachama atawasilisha fomu ya maombi pamoja na hati zifuatazo:-

(i) Barua ya maombi ya mafao ya uzazi.
(ii) Kivuli cha kadi ya Uanachama wa Mfuko.
(iii) Kivuli cha kizazi Hai cha mtoto
(iv) Kivuli cha gamba la kliniki la mama.
(v) Nakala ya barua ya likizo ya uzazi kutoka kwa mwajiri.
(vi) Picha moja ya aina ya pasi ya kusafiria.
(vii) Hati nyingine zozote zinazoweza kuthibitisha maombi hayo.
(viii) Nambari ya hesabu ya mwanachama(bank Account)

MAOMBI YA MAFAO YA UZAZI YASIYOLIPWA

Hakutakuwa na malipo ya mafao ya uzazi kwa mwanachama ambae atajifungua na kufariki wakati wa kujifungua.

Mfuko hautolipa mafao ya uzazi kwa mwanachama ambae atajifungua akiwa nje ya nchi.

Mfuko hautolipa mafao ya uzazi kwa mwanachama ambae haikutimia miezi 36 tokea kulipwa mafao ya awali.

Mfuko hautolipa mafao ya uzazi kwa mwanachama ambae atawasilisha maombi yake baada ya siku 90 tokea kujifungua.

KIWANGO CHA MALIPO YA MAFAO YA UZAZI

Baada ya kufanyika kwa tathmini ya uhai wa Mfuko mwaka 2016 Mfuko umebadilisha kiwango cha malipo ya mafao ya uzazi kwa kukiongeza kwa asilimia 200 kwa sasa. Kiwango hicho kita gawanywa mara mbili iwapo mwanachama atawasilisha maombi yake kabla ya kujifungua.

Kwa mwanachama atakaejifungua watoto mapacha atalipwa asilimia 100 ya kiwango hicho jumlisha na nusu ya awamu ya mwanzo.

Izingatiwe kwamba malipo haya yamezingatia wastani wa mshahara wa mwanachama wote wa ZSSF.

"Mafao ya uzazi ni faraja kwa mama na mtoto"

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:

Mkurugenzi Mwendeshaji
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar
S.L.P: 2716 Zanzibar – Tanzania
Simu: +255 24 2230342
Faksi: +255 24 2232820
Barua pepe: info@zssf.or.tz
Tovuti: www.zssf.or.tz
Kilimani Mnara wa Mbao

PEMBA
S.L.P: 293
Simu: +255 24 52050 I Faksi: +255 24 52050
Chakechake
Barua pepe: info@zssf.or.tz
Tovuti: www.zssf.or.tz

MKOA WA KUSINI UNGUJA
S.L.P: 2716, Zanzibar -Tanzania,
Simu: +255 (0)773 232 835,
Barua pepe: info@zssf.or.tz
Tovuti: www.zssf.or.tz
Kitogani

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA
S.L.P: 2716, Zanzibar -Tanzania,
Simu: +255 (0)773 336 477,
Barua pepe: info@zssf.or.tz
Tovuti: www.zssf.or.tz
Kinduni



© Unicef Germany/ Diana Mrazikova/2013

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

MUONGOZO WA MAFAO YA UZAZI